

Inter-Religious Council for Peace Tanzania



Religions for Peace



Maazimio ya Baraza la Viongozi wa Dini Mbalimbali Kitaifa Kuhuisha Mchakato wa Katiba Mpya Yaliyofanyika Katika Hoteli ya Golden Tulip, Dar es salaam Aprili 11 hadi 12, 2017

Utangulizi

Dhumuni kuu la kikao hiki ambacho kimehusisha viongozi ishirini na tano (25) wakiwakilisha mitandao ya dini mbalimbali ilikuwa kujifunza zaidi na kujadiliana juu ya mchakato wa kupata katiba mpya na kujikumbusha mwenendo na ulipofikia.

Mambo tuliyojifunza ni pamoja na; historia ya mabadiliko ya katiba nchini, mchakato mzima wa upatikanaji wa katiba mpya, maudhui ya rasimu ya pili ya katiba na katiba pendekezwa. Kwa mujibu wa mafunzo hayo yaliyoratibiwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu tumebaini miongoni mwa sababu za msingi zilizopelekea kusita kwa mchakato wa kupata katiba mpya ni kuwepo kwa muingiliano wa hatua ya kura ya maoni na maandalizi ya uchaguzi mkuu 2015 ambapo Tume ya Uchaguzi ilishindwa kuratibu mambo mawili makubwa kwa wakati mmoja: maandalizi ya kura za maoni na uboreshaji wa daftari la wapiga kura.


Kwa kutambua hayo tumeazimia yafuatayo:

- i. Tumeonelea kwamba mwenye mamlaka ya mwisho katika maamuzi ya kuendelea na mchakato ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo tunamsihi Rais akamilishe mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya mapema kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ili kuepusha muingiliano kama uliojitokeza awali.
- ii. Pamoja na kutambua mapungufu yaliyopo katika Katiba Pendekezwa, tumekubaliana kushauri mchakato kusonga mbele kwa hatua ya kurekebisha sheria za mchakato (Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya Kura ya Maoni) na hatimaye wanananchi kupiga kura ya maoni.

Ni matumaini yetu kuwa ushauri huu utazingatiwa ili kuenzi maamuzi ya kuwa na katiba inayotokana na wananchi pamoja na kurasimisha jitihada za viongozi na wananchi katika kukuza ustawi wa jamii na kudumisha Amani nchini.

Katiba ni Yetu, Taifa ni Letu. Sote Tuhusike!

Kwa niaba ya wajumbe,


Mchungaji, Canon Goda

Mkurugenzi Mtendaji – IRCPT

Interreligious Council for Peace
Religions for Peace
Tanzania

P.O. Box 5324, Dar es Salaam